# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

***(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)***

**Sehemu ya CXXXIV Nam. 7379** **01 AGOSTI , 2025** **Bei Shs. 5000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*


**YALIYOMO** Ukurasa


Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar, Nam.7 ya 1997
Kanuni za Tume ya Utangazaji Zanzibar (Huduma za Utangazaji wakati wa Uchaguzi)
[chini ya vifungu vya 29]...........................................................................1011


**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la sheria lililotajwa hapo chini limetengenezwa katika Gazeti Rasmi hili

Tangazo la Sheria.

Nam:72 :- Kanuni za Tume ya Utangazaji Zanzibar (Huduma za Utangazaji wakati wa Uchaguzi)

---

**SHERIA YA TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1997**

---

**KANUNI ZA TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR (HUDUMA ZA UTANGAZAJI WAKATI WA UCHAGUZI)**

**[Chini ya kifungu cha 29]**

---

**MPANGILIO WA KANUNI**

**KANUNI** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

SEHEMU YA PILI
UTANGAZAJI WA HABARI

4. Wajibu wa kuripoti habari.
5. Uwasilishaji wa vipindi.
6. Utambulisho wa haki za mhojiwa.
7. Matumizi ya simu na mitandao ya kijamii katika vipindi.
8. Umma kushiriki katika midahalo ya kisiasa.
9. Mdahalo wa kisiasa.
10. Mtoa huduma wa maudhui kuhakikisha ulinganifu kwenye mdahalo.
11. Haki ya kujibu.
12. Mtoa huduma wa maudhui ya mtandaoni.

SEHEMU YA TATU
UGAWAJI WA MUDA WA KURUSHA MATANGAZO

13. Kutenga muda wa vipindi vya uchaguzi.
14. Utaratibu wa kuzingatia katika kutoa muda wa kwenda hewani.
15. Wajibu wa mtoa huduma za maudhui.
16. Matangazo ya kisiasa.
17. Utoaji wa maoni ya wapiga kura.
18. Mgongano wa maslahi.
19. Utangazaji siku ya kupiga kura.
20. Kutangaza matokeo ya uchaguzi.

SEHEMU YA TANO
MALALAMIKO NA KUKATA RUFAA

21. Utoaji wa malalamiko.
22. Taratibu za utoaji wa malalamiko Tume.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MENGINEYO

23. Makosa na adhabu.
24. Uwezo wa kumaliza kosa.
25. Utaratibu wa kumaliza kosa.
26. Rufaa.

JADWELI

**TANGAZO NAM. 72**

**SHERIA YA TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1997**

---

**KANUNI ZA TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR (HUDUMA ZA UTANGAZAJI WAKATI WA UCHAGUZI)**

**[Chini ya kifungu cha 29]**

---

**KWA UWEZO** niliopewa chini ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Tume ya Utangazaji, Nam. 7 ya 1997, **Mimi, TABIA MAULID MWITA**, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, natunga kanuni zifuatazo:

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Tume ya Utangazaji Zanzibar (Huduma za Utangazaji Wakati wa Uchaguzi), 2025 na zitaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi. Jina fupi na kuanza kutumika.

**2**. Kanuni hizi zitatatumika kwa ajili ya kumuongoza mtoa huduma za maudhui wa redio na televisheni, wakiwemo watoaji wa maudhui ya mitandaoni na mawakala wa habari wanaofanya kazi Zanzibar wakati wa uchaguzi mkuu, uchaguzi mdogo, uchaguzi wa marudio na kura za maoni kwa nafasi zote za wagombea. Matumizi.

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokua kama maelezo yatahitaji vyenginevyo: Ufafanuzi.

"chama" au "chama cha siasa" maana yake ni chama kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Nam. 5 ya 1992;

"hotuba za chuki" maana yake ni maelezo yoyote yanayotolewa kwa njia ya sauti, ishara, maandishi au picha yanayodhalilisha, kukashifu au kushusha hadhi ya mtu au kikundi kwa msingi wa rangi, ukabila, dini au ulemavu;

"huduma ya utangazaji" maana yake ni huduma za maudhui yanayosafirishwa kwa kutumia njia za mawasiliano ya eletroniki ambapo usafirishaji huo unakusudiwa kupokelewa moja kwa moja na umma;

"huduma za maudhui" maana yake ni huduma za utangazaji zinazotolewa kwa njia ya matamshi au sauti nyengine, maandishi au picha, zikiwa tulivu au jongevu isipokuwa pale ambapo zinatangazwa kwa njia ya mawasiliano binafsi;

"jukwaa mtandaoni" maana yake ni kituo cha intaneti ambapo watu wanaweza kupata habari, burudani, elimu, dini au taaarifa nyengine kupitia televisheni, redio, mtandao wa kijamii na blogu za mtandaoni;

"kipindi" maana yake ni kipindi chenye maudhui mubashara au yaliyorekodiwa kinachojumuisha picha, sauti, michoro au vyote, kinachorushwa kwa madhumuni ya kufikisha ujumbe kwa umma;

"kipindi cha chama cha siasa" maana yake ni kipindi chenye maudhui ya kisiasa kinachoshawishi watu kufanya uamuzi na uteuzi kwa wagombea wakati wa uchaguzi;

"maudhui ya mtandaoni" maana yake ni maudhui yanayotangazwa kwa umma kupitia tovuti za intaneti, programu tumizi za kompyuta, majukwaa, blogu, tovutiblogu, blogu ndogondogo, akaunti ya umma, zana za ujumbe mfupi wa papo hapo, matangazo ya moja kwa moja mtandaoni, mikusanyiko na majukwaa mengine yanayohusiana nayo;

"malalamiko" maana yake ni maelezo yoyote ya kutoridhika na bidhaa au huduma inayotolewa kwa watumiaji, mwenendo mbaya katika mchakato wa utoaji wa huduma, au habari kutoendana na maadili ya utangazaji;

"matangazo ya kisiasa" maana yake ni matangazo yaliyolipiwa na yanayokusudia kuendeleza maslahi ya chama cha siasa chochote;

"matangazo ya uchaguzi" maana yake ni muda wa vipindi vya televisheni na redio vinavyohusu vyama vya siasa ambavyo wagombea hunadi sera zao kwa wapiga kura;

"mgombea" maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa na Tume ya Uchaguzi kugombania nafasi ya Rais wa Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani;

"mitandao ya kijamii" maana yake ni tovuti au programu za komyuta ambazo zinawezesha watu kuwasiliana na kubadilishana taarifa kupitia intaneti kwa kutumia kompyuta, simu ya mkononi, kishkwambi au kifaa chochote cha mawasiliano;

"mlalamikaji" maana yake ni mtu yeyote aliyewasilisha malalamiko Tume dhidi ya habari iliyorushwa hewani na mtoa huduma ya maudhui ya utangazaji yaliyoathiri maslahi yake;

"mtoa huduma za maudhui" maana yake ni mtu aliyepewa leseni ya kutoa huduma ya utangazaji chini ya Sheria;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar, Nam. 7 ya 1997;

"Tume" maana yake ni Tume ya Utangazaji Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria;

"Tume ya Uchaguzi" maana yake ni Tume ya Uchaguzi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar au Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"uchaguzi" maana yake ni mchakato wa kuchagua mtu kwa nafasi ya Rais wa Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mbunge, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani kwa kupiga kura, unaosimamiwa na Tume ya Uchaguzi;

"wakati wa uchaguzi" maana yake ni kipindi kuanzia uteuzi wa wagombea hadi kutangazwa kwa matokeo au kama itakavyoelekezwa na Tume ya Uchaguzi; na

"Waziri" maana yake ni waziri anayehusika na habari.

## SEHEMU YA PILI
## UTANGAZAJI WA HABARI

Wajibu wa kuripoti habari.

**4**. Mtoa huduma za maudhui atahakikisha kuwa:

(a) utangazaji wa habari zote wakati wa uchaguzi unaripotiwa na kuwasilishwa bila ya upendeleo na kwa namna ya uadilifu bila kuonesha mtazamo binafsi wa kituo cha utangazaji;

(b) shughuli za utangazaji wa habari, ikijumuisha majadiliano ya watu na mdahalo wa umma, unatendewa haki kwa maslahi ya wote;

(c) anatoa haki kwa uwiano sawa na usahihi, na anaripoti matukio ya kisiasa kwa uadilifu na haki, kwa vyama vyote wakati wa uchaguzi;

(d) taarifa ya chama cha siasa iliyopo kwenye habari ni ya kweli, na inayofuata misingi na maadili ya uandishi wa habari;

(e) habari za chama cha siasa zinatangazwa bila ya kuongezwa chochote na mtangazaji;

(f) hatotangaza hotuba yoyote ya chuki, uchochezi, kashfa, uzushi na jambo lolote lenye kuleta mgawanyiko katika jamii;

(g) ripoti kuhusu utaratibu wa uchaguzi na nafasi za wagombea wa vyama vya siasa ni sahihi na haziegemei upande wowote;

(h) taarifa za utaratibu wa uchaguzi zinakusudia kusisitiza umuhimu wa uchaguzi na kuhamasisha ushiriki wa wananchi wote katika utaratibu wa uchaguzi; na

(i) habari zinajumuisha masuala yanayonufaisha wananchi na sio kueleza tu matukio ya vyama vya siasa au wagombea.

Uwasilishaji wa vipindi.

**5**. Mtoa huduma za maudhui atahakikisha vipindi na uwasilishwaji wake:

(a) unafuata sera, sheria, kanuni na miongozo inayosimamia uendeshaji wa shughuli za huduma za utangazaji;

(b) hauhusishi upotoshaji wa taarifa binafsi ya mgombea au mtu mwengine, au maoni yasiyofaa juu ya sifa za mtu yeyote;

(c) hauhusishi maoni ya kisiasa yaliyojengeka katika ubaguzi wa kikabila, rangi, ulemavu, dini, imani, jinsia au eneo analotoka mtu;

(d) usiwe na viashiria vya lugha ya kukashifu, uvunjifu wa sheria au sauti inayoweza kusababisha vurugu, uchochezi au uasi;

(e) hautohusisha utoaji wa maoni yanayoweza kuumiza hisia za mtu kutokana na jinsia, jinsi, kabila, rangi, tabaka, imani au eneo analotoka;

(f) una maudhui ya siasa ambayo vyama vinataka kunadi sera, mipango na malengo yake;

(g) una maudhui ya siasa yatakayobainishwa kwa uthabiti na hayatotangazwa kwa namna ambayo inaweza kuipotosha hadhira na kuamini kwamba kipindi hicho kina mtazamo mwengine wowote;

(h) unafuata miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Uchaguzi; na

(i) unaepuka hisia ya kupendelea upande mmoja katika vipindi vyote na hayataathiriwa na maslahi ya kisiasa.

Utambulisho wa haki za mhojiwa.

**6**. Mtoa huduma za maudhui anapofanya mahojiano katika vipindi vya kisiasa atahakikisha kuwa:

(a) muhojiwa anayezungumza kwa niaba ya chama amepata ridhaa ya chama husika;

(b) hakuna muhojiwa atakayehojiwa moja kwa moja bila ya ridhaa yake;

(c) msimamizi wa mjadala wa vipindi hivyo anasimamia na anahakikisha kuwa muhojiwa anajikita katika mada iliyochaguliwa;

(d) msimamizi wa mjadala anatoa vipindi ambavyo havipotoshi kwa lugha ya mzaha, matusi au kejeli;

(e) mahojiano yaliyohaririwa au kufupishwa hayaathiri mazungumzo yaliyofanyika au kubadili maoni ya wahojiwa na michango yao; na

(f) mahojiano yasihaririwe kwa nia ya kupotosha ukweli au kuonekana yanamuhusisha mchangiaji na hoja fulani ambazo hakubaliani nazo.

Matumizi ya simu na mitandao ya kijamii katika vipindi.

**7**.-(1) Mtoa huduma za maudhui atahakikisha kuwa:

(a) kutakuwa na usawa, uaminifu na uadilifu wa kutopendelea katika utaratibu wa vipindi vya kupiga simu moja kwa moja au kupitia mitandao ya kijamii;

(b) anachukua hatua muhimu kuhakikisha kwamba hakuna mpiga simu au mchangiaji kupitia mitandao ya kijamii anayeshiriki katika vipindi vya kisiasa au vipindi vyengine kwa kukiuka Sheria, kanuni na miongozo iliyotolewa na Tume;

(c) taarifa binafsi za wachangiaji kupitia simu au mitandao ya kijamii zinalindwa;

(d) simu zinazopigwa zipitie katika mchakato wa kuchunguzwa kwanza kabla ya kurushwa hewani katika kipindi;

(e) muwasilishaji wa kipindi anachukuwa tahadhari ya kutosha anapomuhoji mtu kwa njia ya simu na kutoruhusu kwa njia yoyote kurusha kauli ambazo zinaweza kudhoofisha au kuteza utu wa mtu;

(f) taarifa za mchangiaji kupitia mitandao ya kijamii zinachujwa kabla ya kurushwa hewani;

(g) vipindi vyote vinavyorushwa mubashara vitawasilishwa kwa uangalifu na kuhakikisha kwamba taarifa zote ni sahihi na hazipotoshi ukweli uliopo;

(h) watazamaji, wasikilizaji, wachangiaji kupitia mitandao ya kijamii na wanaopiga simu wakati wa kipindi na kurushwa hewani moja kwa moja, wanahudumiwa kwa heshima, uadilifu na usawa; na

(i) vipindi vinavyoshirikisha hadhira kwa kuruhusu watu kuchangia kupitia simu havitaruhusiwa kupandikiza taarifa ambayo haiwezi kuthibitishwa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1)(d) ya kanuni hii, mchakato wa uchunguzi utajumuisha ucheleweshaji wa sekunde tatu hadi tano kutoka studio hadi kituo cha kurushia matangazo.

Umma kushiriki katika midahalo ya kisiasa.

**8**.-(1) Mtoa huduma wa maudhui atatoa fursa kwa umma kushiriki katika midahalo ya kisiasa inayohusu masuala ya uchaguzi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, washiriki katika vipindi hivyo lazima wawe wawakilishi wa mitazamo na sekta mbali mbali zilizopo katika jamii.

Mdahalo wa kisiasa.

**9**.-(1) Mdahalo wa kisiasa utahusisha msimamizi wa mdahalo na angalau mwakilishi mmoja kutoka katika kila chama cha siasa ukijadili suala au mada inayohusika.

(2) Mshiriki wa mdahalo atazungumza na mtazamaji au msikilizaji juu ya ilani au sera ya chama husika.

(3) Endapo upande mmoja utashindwa kushiriki katika mdahalo unaohusisha vyama viwili, kipindi hicho kitaghairishwa mpaka hapo ushiriki wa vyama vyote viwili utakapopatikana.

(4) Endapo zaidi ya vyama viwili vimehusishwa katika mdahalo, na ikiwa hakuna sababu ya msingi ya kutokuwepo kwa mwakilishi wa chama fulani ndani ya saa ishirini na nne kabla ya kipindi kuanza, mdahalo huo utaendelea na mtangazaji atauarifu umma chama ambacho hakikushiriki.

(5) Endapo mtangazaji wa kipindi au mwendesha mjadala anapokutana na wanasiasa wakati anatekeleza majukumu yake ya kitaalamu, hatodhihirisha msimamo wa chama chake.

Mtoa huduma wa maudhui kuhakikisha ulinganifu kwenye mdahalo.

**10**. Mtoa huduma wa maudhui, ili kutenda usawa kwa hadhira, atahakikisha kuwa:

(a) kila mgombea anaalikwa kuleta idadi sawa ya wafuasi wake kulingana na mahitaji ya kituo, isipokuwa mgombea anaweza kuleta idadi pungufu ya wafuasi akiona inafaa;

(b) wafuasi wa vyama wanatenganishwa kulingana na vyama ili kumuwezesha msimamizi wa mjadala kuwatumia bila ya upendeleo;

(c) msimamizi wa mjadala hatoi muhtasari, suluhisho au ufafanuzi wakati au mwishoni mwa mjadala;

(d) anavitendea usawa vyama vyote vya siasa au wagombea na kuwezesha ushiriki sawa kwa wote; na

(e) haruhusu washiriki walioalikwa katika midahalo ya kisiasa kukejeli mifumo ya uchaguzi.

Haki ya kujibu.

**11.**-(1) Mtoa huduma za maudhui atatoa haki ya kujibu kwa chama cha siasa au mgombea pale ambapo taarifa iliyotangazwa si sahihi au ina muelekeo wa chuki na imejikita katika kupotosha ukweli.

(2) Fursa ya kujibu iliyotolewa chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, itatolewa ndani ya saa ishirini na nne katika kipindi cha kiwango na hadhira sawa.

Mtoa huduma wa maudhui ya mtandaoni.

**12**. Mtu yeyote anayeishi ndani au nje ya Zanzibar anayeandaa maudhui ya mtandaoni yanayokusudiwa kutumika Zanzibar katika kipindi cha uchaguzi:

(a) atasajiliwa kwa mujibu wa Sheria;

(b) atafuata ipasavyo Sheria, miongozo pamoja na kanuni zote zilizotolewa na Tume na Tume ya Uchaguzi;

(c) atahakikisha maelezo na taarifa zinazotolewa katika jukwaa mtandaoni yawe sahihi, ya ukweli, na yatolewe na muwakishi aliyeridhiwa na chama husika;

(d) atafanya jitihada za kuhariri majadiliano yanayoelekea kuumiza hisia za mtu yeyote kwa kutumia lugha ya kashfa ambayo inaweza kuchochea vurugu, uasi au uvunjifu wa amani;

(e) atachukua tahadhari kuhakikisha usahihi katika kutangaza matokeo yoyote ya uchaguzi au kura za maoni kama yalivyotolewa na Tume ya Uchaguzi.

## SEHEMU YA TATU
## UGAWAJI WA MUDA WA KURUSHA MATANGAZO

Kutenga muda wa vipindi vya uchaguzi.

**13**.-(1) Mtoa huduma za maudhui atatenga muda wa kutangaza utakaotumika kutoa vipindi vya vyama vyote vya siasa.

(2) Wakati wa uchaguzi, vipindi vya vyama vya siasa vitatangazwa kulingana na mpangilio wa vipindi ulioidhinishwa na Tume.

(3) Mwakilishi wa chama ataeleza ilani au sera ya chama husika kwa muda usiozidi dakika thelathini.

(4) Muda wa kurusha vipindi vya uchaguzi utakuwa umegawanywa kwa vyama mbalimbali vinavyoshindana katika uchaguzi kulingana na utaratibu uliowekwa na mtoa huduma za maudhui na kuidhinishwa na Tume.

(5) Mtoa huduma za maudhui atatunza daftari la kumbukumbu linaloonesha ugawaji wa muda kwa kila chama, tarehe, jina la kipindi na maelezo mengine kama yanavyohitajika.

(6) Wagombea na vyama vya siasa watapewa fursa sawa za muda wa kwenda hewani usiolipiwa.

Utaratibu wa kuzingatia katika kutoa muda wa kwenda hewani.

**14**.-(1) Mtoa huduma za maudhui yuko huru kuuza muda wa kwenda hewani kwa lengo la kutangaza mikutano ya kampeni za kisiasa.

(2) Kipindi cha matangazo ya biashara au mdhamini hakiruhusiwi kuingia katikati wakati wa kipindi cha chama cha siasa kinarushwa hewani.

## SEHEMU YA NNE
## UTANGAZAJI WAKATI WA KAMPENI ZA UCHAGUZI

Wajibu wa mtoa huduma za maudhui.

**15**.-(1) Mtoa huduma za maudhui, wakati wa kampeni za kisiasa, atazingatia kuwa:

(a) wawakilishi wa chama wanaoshiriki katika kipindi cha chama cha siasa wameteuliwa na chama husika;

(b) anafuata Sheria, kanuni na maadili ya utangazaji;

(c) suala la utangazaji wa masuala ya kisiasa linafanyika kwa usawa kati ya chama kimoja na chengine, isipokuwa pale ambapo suala hilo limechaguliwa na chama husika;

(d) wachambuzi waliopendekezwa kuangalia mitazamo ya vyama vya siasa ni wabobezi katika mada husika kutoka taasisi zisizofungamana na chama cha siasa chochote; na

(e) anatofautisha kauli na vitendo vya viongozi na watumishi wa Serikali katika kipindi cha kampeni kuwa ni za kiutumishi au za kisiasa.

(2) Mtoa huduma za maudhui atasita kutoa matangazo ya uchaguzi wa vyama vya siasa baada ya kipindi cha kampeni kumalizika.

(3) Tume inaweza kutoa maelekezo mengine yoyote ya urushaji wa vipindi wakati wa uchaguzi.

Matangazo ya kisiasa.

**16**.-(1) Mtoa huduma za maudhui atahakikisha kuwa:

(a) sura na sauti za wafanyakazi wa kituo cha utangazaji hazitatumika katika matangazo ya kisiasa;

(b) matangazo ya kisiasa yanafuata misingi ya heshima, stara, staha na maadili;

(c) kiasi cha muda uliotengwa kwa ajili ya matangazo ya kisiasa na kiwango cha kulipia kitalingana kwa vyama vyote na kwa wagombea wote;

(d) anatoa nafasi kwa vyama vya siasa kutangaza matangazo ya kisiasa kulingana na taratibu za chombo husika; na

(e) anaandaa utaratibu wa wazi wa kugawa muda wa kurusha matangazo utakaotolewa kwa kila chama au mgombea.

(2) Mtoa huduma za maudhui anaweza kutangaza tangazo la kisiasa la kulipia muda wowote katika wakati wa uchaguzi ambalo:

(a) ni la kweli na lenye taarifa yenye kueleweka kwa asili yake; na

(b) litahusisha jina la chama, mgombea, jina la mzungumzaji, muda na mahali pa tukio.

(3) Mtoa huduma za maudhui hatoweka muziki, nyimbo, misemo au kauli mbiu itakayodokeza masuala ya kisiasa, kabla au mara tu baada ya tangazo la kisiasa lililolipiwa.

(4) Mtoa huduma za maudhui baada ya kutoa kipindi au tangazo la kisiasa la chama kimoja atapitisha muda wa angalau dakika tano kabla ya kutangaza kipindi au tangazo la kisiasa la chama chengine au mgombea.

(5) Mtoa huduma za maudhui atatoa utaratibu wa uandaaji wa vipindi, matangazo na taarifa rasmi kwa vyama vya siasa utakaojuilishwa kwa vyama vya siasa na nakala kuwasilishwa Tume, utakaozingatia:

(a) ubora wa sauti, picha na video zinazotumika;

(b) muda wa vipindi; na

(c) viwango vya kiufundi.

(6) Mtoa huduma za maudhui ataendeleza utaratibu wa uwazi katika kuhakikisha kuwa matangazo ya kisiasa na matangazo ya chama ya uchaguzi hayahaririwi au kufanyiwa marekebisho bila ridhaa ya chama cha siasa na mgombea isipokuwa kama marekebisho hayo ni ya matangazo au habari inayokwenda kinyume na sheria au muongozo wowote wa uchaguzi, au haiendani na viwango vya kiufundi vinavyotakiwa.

(7) Endapo chama cha siasa au mgombea amekataa kufanyiwa uhariri au marekebisho katika tangazo au kipindi kinachokwenda kinyume na sheria au muongozo wowote wa uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo (6) ya kanuni hii, mtoa huduma za maudhui ana haki ya kukataa kutangaza tangazo au kipindi hicho.

(8) Gharama za viwango vya matangazo na taratibu ikijumuisha kiasi cha punguzo na bonasi iliyowekwa zitakuwa sawa kwa vyama na wagombea wote.

(9) Mtoa huduma za maudhui atahakikisha mgombea anatangaza kwa kuomba kura tu, na anaweza kutumia jina la chama, sera na ilani.

(10) Mtoa huduma za maudhui atalipwa fidia na chama cha siasa au mgombea dhidi ya uharibifu au hasara iliyotokea ambayo ni matokeo ya makubaliano yaliyotokana na utayarishaji wa habari au matangazo.

Utoaji wa maoni ya wapiga kura.

**17.**-(1) Mtoa huduma za maudhui atahakikisha utangazaji wa maoni ya wapiga kura unafanyika kwa tahadhari na:

(a) kuuarifu umma juu ya taasisi iliyohusika kukusanya na kutoa maoni; na

(b) kutangaza muda yaliyopatikana maoni, ukubwa wa sampuli na baadhi ya dosari zilizojitokeza.

(2) Matokeo ya maoni kwa njia ya ujumbe wa simu na mitandao ya kijamii yaliyokusanywa na mtoa huduma za maudhui kutoka kwa hadhira hayatachukuliwa kuwa ni matokeo ya kisayansi na hayatotangazwa.

(3) Matokeo ya maoni hayatotangazwa ndani ya siku thelathini kabla ya siku ya kupiga kura.

Mgongano wa maslahi.

**18**.-(1) Mfanyakazi wa kituo cha utangazaji hatoruhusiwa kutangaza au kufanya kazi ya uhariri akiwa ana mgongano wa kimaslahi.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, mfanyakazi wa kituo cha utangazaji atahesabika kuwa ana mgongano wa maslahi ikiwa:

(a) ni mwenye wadhifa wa kisiasa au mtumishi wa chama cha siasa;

(b) ameshiriki katika shughuli za utangazaji akiwa ni mgombea; au

(c) amevaa nguo yoyote yenye alama, nembo ya chama cha siasa au picha ya mgombea.

(3) Endapo mfanyakazi wa kituo cha utangazaji atakuwa mgombea au ataajiriwa na mgombea wa kisiasa au chama cha siasa, atachukua likizo au kusitisha ajira yake kwenye kituo cha utangazaji katika kipindi cha uchaguzi.

Utangazaji siku ya kupiga kura.

**19**.-(1) Mtoa huduma ya maudhui, mara baada kufungwa rasmi kampeni hadi kumalizika upigaji kura, atahakikisha kuwa:

(a) hatangazi kipindi chochote cha matangazo ya kisiasa au matangazo ya uchaguzi;

(b) anasita kutumia maoni yake binafsi kama sehemu ya taarifa zinazohusiana na uchaguzi;

(c) anaripoti matukio na maelezo sahihi ya mashuhuda na mahudhurio katika vituo vya kupigia kura anapotaka kuripoti masuala ya uchaguzi;

(d) mahojiano na waangalizi na wasimamizi wa uchaguzi yanaweza kutumika katika kudumisha uwazi kwenye zoezi la upigaji kura; na

(e) anaepuka kupendelea upande wowote na kutoa ripoti za kukisia au zisizo na uhakika.

(2) Mtoa huduma za maudhui hatoruhusiwa kutangaza kwa umma mambo yafuatayo katika kipindi chote cha uchaguzi, siku yoyote ya kupiga kura hadi kumalizika kwa zoezi la upigaji kura:

(a) mijadala na uchambuzi wa masuala ya uchaguzi na maoni ya uchaguzi;

(b) kutoa matokeo yoyote ya upigaji kura katika jimbo la uchaguzi kabla ya kutangazwa na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo husika;

(c) kutotoa aina yoyote ya matangazo kwa njia ya picha au video yenye kutoa taswira ya ushindi kwa mgombea fulani wakati wa kuhesabu kura;

(d) kutoa matangazo yoyote ya kisiasa, habari za kisiasa, au vipindi vyovyote vya uchaguzi vilivyoandaliwa na mgombea au kwa niaba yake, chama cha siasa au mtu mwengine au chombo chochote;

(e) kutoa matokeo ya kura zilizopita; na

(f) kutangaza maoni au chaguo la mpiga kura mshiriki.

**20**. Mtoa huduma za maudhui atahakikisha kuwa: Kutangaza matokeo ya uchaguzi.

(a) hatangazi kwa aina yoyote matokeo ya uchaguzi ambayo hayajatolewa na Tume ya Uchaguzi; na

(b) hatangazi maoni yenye kuashiria uchochezi wenye kuleta vurugu, chuki au uvunjifu wa amani.

## SEHEMU YA TANO
## MALALAMIKO NA KUKATA RUFAA

**21**.-(1) Malalamiko yatawasilishwa na mlalamikaji kwa maandishi, kwa mtoa huduma za maudhui ndani ya muda wa saa arobaini na nane tokea kutangazwa kwa suala linalolalamikiwa. Utoaji wa malalamiko.

(2) Mtoa huduma za maudhui atayafanyia kazi na kuyatolea uamuzi malalamiko yatakayowasilishwa kwake ndani ya muda wa saa sabini na mbili tokea kupokea malalamiko.

(3) Endapo mlalamikaji hakuridhika na uamuzi uliotolewa au hakuna uamuzi uliotolewa na mtoa huduma za maudhui katika kipindi kilichoainishwa, atawasilisha malalamiko Tume kwa maandishi, ndani ya muda wa saa arobaini na nane baada ya uamuzi kutolewa au kushindwa kutolewa.

**22**.-(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria, malalamiko rasmi juu ya vipindi vya uchaguzi yatawasilishwa Tume kwa maandishi, na yahusishe: Taratibu za utoaji wa malalamiko Tume.

(a) jina la kipindi;

(b) chama au mgombea aliyeonekana kwenye tangazo;

(c) kituo cha redio au chaneli ya televisheni iliyoonyesha tangazo au kipindi;

(d) tarehe na muda wa kutangazwa;

(e) vifungu vya Kanuni hizi vinavyodaiwa kuvunjwa na sababu za kuvunjwa; na

(f) unafuu unaotarajiwa kupatikana.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

**23**.-(1) Mtoa huduma za maudhui ambaye: Makosa na adhabu.

(a) amekiuka wajibu wa kuripoti habari;

(b) ametumia lugha ya kukashifu, inayoashiria ubaguzi wa aina yoyote , mzaha, matusi , kejeli;

(c) ametoa hotuba za chuki;

(d) amepotosha taarifa binafsi za mgombea au mtu mwengine;

(e) amekiuka miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume ya Uchaguzi;

(f) amemuhoji mtu au kurusha mahojiano katika vipindi vya siasa bila ya ridhaa yake;

(g) ametangaza au amesambaza kwa mtu mwengine taarifa binafsi za wachangiaji kupitia simu na mitandao ya kijamii;

(h) hajatoa usawa na uadilifu wakati wa vipindi vya midahalo ya kisiasa;

(i) amekataa kutoa haki ya kujibu;

(j) ametangaza vipindi vya siasa bila ya kufuata mpangilio wake wa vipindi ulioindhinishwa na Tume;

(k) ametoa matangazo ya uchaguzi wa vyama vya siasa baada ya kipindi cha kampeni kumalizika;

(l) amemruhusu mtumishi wa kituo cha utangazaji kutangaza au kufanyakazi ya uhariri akiwa ana mgongano wa kimaslahi;

(m) ametumia sura na sauti za wafanyakazi wa kituo cha utangazaji katika matangazo ya kisiasa;

(n) ametangaza matokeo ya maoni ya uchaguzi ndani ya siku thelathini kabla ya kupiga kura;

(o) ametangaza matangazo ya kisiasa au matangazo ya uchaguzi siku ya kupiga kura;

(p) amekataa kufuata maelekezo yotote ya Tume kuhusiana na kuripoti habari za uchaguzi,

ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Uwezo wa kumaliza kosa.

**24**. Endapo mtoa huduma za maudhui amekiuka masharti ya Kanuni hizi, Katibu mtendaji anaweza, kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa chini ya Kanuni hizi, kumaliza kosa lililotendwa.

Utaratibu wa kumaliza kosa.

**25**.-(1) Kwa kuzingatia uwezo chini ya masharti ya kanuni ya 24 ya Kanuni hizi, Katibu Mtendaji atampa mtu huyo, notisi iliyoainishwa chini ya Jadweli la Kanuni hizi, itakayomtaka mtu huyo kulipa faini kulingana na kosa alilotenda.

(2) Notisi chini ya masharti ya kanuni ndogo (1) ya kanuni hii, itaanisha:

(a) jina na anwani ya mtu;

(b) tarehe na eneo la kosa lilipotokea

(c) kosa lililoshutumiwa kutendwa;

(d) eneo na muda ambao kosa limetendwa;

(e) kiwango cha faini kitakachotakiwa kulipwa kwa kosa hilo;

(f) muda na namna ambayo faini italipwa; na

(g) taarifa au maelezo mengine yoyote yanayohusiana na kosa hilo kama Katibu Mtendaji atakavyoona muhimu.

(3) Mtu aliyepewa notisi chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, ndani ya siku saba kutoka siku ambayo notisi imepokelewa, atalipa kiwango cha faini kwa Tume.

(4) Endapo mtu ambaye amepewa notisi chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, atashindwa kulipa kiwango cha faini kilichoainishwa ndani ya muda wa notisi, Katibu Mtendaji ataendelea kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtu huyo.

(5) Endapo mtu atalipa kiwango cha faini kilichoainishwa ndani ya notisi, hakuna hatua za kisheria zitakazochukuliwa kuhusiana na kosa hilo kwa mtu huyo.

**26**. Endapo mtu hajaridhika na uamuzi wa Tume anaweza kukata Rufaa kwa Baraza la Ushindani halali wa Biashara la Zanzibar kwa mujibu wa utaratibu ulioainishwa katika Sheria ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Zanzibar, Nam. 5 ya 2018. Rufaa.

**JADWELI**

**NOTISI YA KUMALIZA KOSA**
**[Chini ya kanuni ya 25(1)]**

**A : TAARIFA ZA ALIYEFANYA VIBAYA**

Jina kamili ..............................................................................................

Tarehe ......................................................................................................

Aina ya kosa lililotendwa ..................................................................

Mahali na wakati wa kosa lililotendwa ...........................................

**B: AINA YA FAINI**

Idadi ya kosa makosa yaliyotendwa ...............................................

Faini ........................................................................................................

Taarifa nyengine (kama zipo) ..........................................................

**C: TAMKO**

Mimi ................................................ natangaza kwamba, taarifa zote zilizomo humu ni za kweli kwa kadri ninavyojua. Kwa hiyo, nitatii notisi hii na nipo tayari kulipa Tsh...................................... kama faini kwa kosa lililoainishwa katika notisi hii.

Jina ...........................................................................

Sahihi.........................................................................

Tarehe.........................................................................

**D: KWA MATUMIZI YA OFISI PEKEE**

Jina la Keshia/wakala anayetoa notisi.............................................
Tarehe ...............................................................

Sahihi ......................................................................................................

Jina la Afisa Msimamizi /wakala anayetoa faini ..........................................

Tarehe ......................................................................................................

Saini ........................................................................................................

Muhuri ......................................................................................................

..................................................
Katibu Mtendaji
Tume ya Utangazaji Zanzibar

**Zimetiwa Saini** Leo tarehe 17th mwezi wa July, 2025.

**MHE. TABIA MAULID MWITA**
**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO**
**ZANZIBAR**

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI - ZANZIBAR 2025